“Yesu Kristo ni yeye Yule jana na leo na hata milele.“

(WAEBRANIA 13:8)

BARUWA YA MUZUNGUKO APRILI 2020

Ujumbe wa saa inayotumwa kupitia Tume ya Mungu

Nina salimu wa amini wote, wandugu wote na wadada Duniani pote na andiko kutoka katika 2 Petro 3:9: *“BWANA hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvmilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotea, bali wote wafikilie toba.“*

Hii ndiyo ahadi: *“Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo“*. (Yohana 14:3)

Tuna shukuru kilindini Mungu kwa na neno la thamani na takatifu, kwa ajili ya Agano la Kale na Jipya, Ijili, baruwa za mitume na kitabu cha Ufunuo. Kila somo la kibiblia imekwesha fundishwa na uwazi kabisa.

Kitu cha muhimukwa waamini wote wa Biblia ilikuwa na ni somo kuhusu kuja kwa pili kwa Kristo. Kwa sasa, hii in na abatana hapo hapo na ujumbe wamwisho iliyo tumwa kwa kuita kutoka, kutegana, na kutayarisha kanisa la Yesu Kristo kwa siku ya utukufu ya kurundi kwa BWANA wetu.

Katika 2 Petro 3:14: “*Kwa hiyo, wapenzi, kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake.“*

Wamitume wa liogozwa kupa waamini maagizo maalum kuhusu somo ya kurundi kwa BWANA wetu. Yohana aliadika ndani ya 1. Yohana 2:28: “*Na sasa, watoto wadogo, kaeni ndani yake, ili kusudi, atakapofunuliwa, mwe na ujasiri, wala msiaibike mbele zake katika kuja kwake.“* Ni ya kushagaza kuona muzingo ambayo Roho wa Mungu aliweka kwa mioyo ya mitume kuhusu umuhimu wa matayarisho kwa ile siku ya utukufu, na nanamna gani walisukumwa kwaku iandika. Hiyo inatumika sana sana kwatu, kwa kuwa tuna juwa sawasawa yakwamba tumefikia lengo kwa wakati unayo fa

mbele ya kurundi kwa Yesu Kristo, kusudi tu ishi matayarisho yatu kwa ukweli.

Maneno yale ambao mtume Paulo aliandika wa mutumishi mwezake Timotheo zinaelekezwa kwangu sana leo, lakini na kwa wandugu wote abao ndani ya uaminifu wana hubiri neno lililofunuliwa na kupana chakula chakiroho: "*Kwamba uilinde amri hii pasipo mawaa, pasipo lawama, hata kufunuliwa kwake BWANA wetu Yesu Kristo…"* (1. Timotheo 6:16) Kwa sasa, mbele ya kurundi ya BWANA, utagazaji unapaswa kuwa wa kibiblia kabisa. Inahusika na kuhubiri Neno la Mungu takatifu bila lawama.

Mutume aliandika kwa shahili la 15 kuhusu kurundi kwa BWANA: *"Ampoko yeye kwa majira yake atakudhihirisha, yeye kwa aliyehimidiwa, mwenye uweza peke yake, MFALME wa waflame…"*

Mungu ameamua kila kitu mapema: Mpango mzima wa okovu, Mambo ambayo igefanyika kwa wakati wa kuja kwa kwanza kwa Kristo, na tena mambo ambayo inafanyika kwa sasa mbele ya kuja kwa pili kwa Kristo. Mtume ageandika: *"Ampoko yeye kwa majira yake atakudhihirisha, yeye kwa aliyehimidiwa…"*

Hiyo ndiye sababu inatumika pia kwa wakati wetu yakwamba Ujumbe utatagulia kuja kwa pili kwa Kristo.

Katika 2. Timotheo 2:15 tuna soma: *"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa hahali neno la kweli."*

Mungu aliwaziya kila kitu kwa kweli. Na tunashukuru; ndiyo, Nina shukuru kwa miaka mingi abayo niliwezeshwa kutaganza Neno la Mungu, bila kujalibu kitu chochote kama matafusiri, kwa kweli, Nilihubiri Neno la Mungu Takatifu.

Ninashukuru sana kwa sababu BWANA aliniamuru kwa mwaka 1980: "Mtumishi wangu, amka na kusoma 2. Timotheo 4". Ni amka, na kushika Biblia yangu na kusoma: "*Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake; Lihubiri Neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya <u>kwa uvumilivu wote na mafundisho</u>.*

Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimun makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo. Bali wewe, uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiliza hudma yako"

Hiyo sura zima inamaana maalum kwangu, tangu siku hiyo. Tuna ona ni maalifa gani iliyo andikwa ndani ya shahili la kwanza. Wakati huo, alifa ya mtume Paulo ilikuwa ikielekea mtumishi mwezake Timotheo. Ndani ya mwaka 1980 BWANA alinipa maandiko hayo. Kisha tunasoma kile Paulo alisema kuhusu hudma yake, na leo hiyo inatumika pia, kasababu ni Ujumbe wa mwisho ambao inatagazwa kupitia utume wa Mungu.

Lakina BWANA alisimama pamoja nami akanitia nguvu, ili kwa kazi yangu ule ujumbe utangazwe kwa utimilifu, hata wasikie mataifa yote; nami nikaokolewa katika kinywa cha simba". (2. Timotheo 4:17)

Tunayo kitu maalum hapa. Paulo aliamini yakwamba mahubir yake ilifunuwa kila kitu ambacho Mungu alikusudia ndani ya mpango wa okovu wake, na kwa hiyo BWANA alimupa nguvu. Haikukuwa kiburi; haikukuwa maoni ya kibinafsi. Ilikuwa utume wa Mungu. Na nguvu zilizo mupewa hazikukuwa za mwana damu, bali ilikuwa kazi ya Roho Mtakatifu.

Paulo alipata kuandika kwa kipeke kuhusu kurundi kwa Yesu Kristo, ndani ya 1 Wakorinto 15, 1 Wathesalonike 4 na katika maandiko mengine kadhaa. Na tunaweza kusoma ndani Tito 1:3: "*…akalifunua neon lake kwa majira yake katika ule ujumbe niliowekewa amana mimi kwa amri yamwokozi wetu Mungu"*.

Tumekwisha soma yakwamba kurundi kwa BWANA kutafanyika muwakati uliotaalishiwa, na hapa kwamba alidhihirisha neno lake kwa wakati uliowekwa. Yote hufanyika katika wakati wetu: Utagazaji wa ujumbe ya neno lililofunuliwa na kurundi kwa BWANA.

Sifa na utukufu kwa BWANA wetu! Aliye tufunulia Neno lake ambao ilitayarishiwa kwa kipindi hiki cha wakati kwa Nabii wake William Branham; vivyo hivyo, Paulo aliweza kushuhundiya kwa wakati wake kuhusu kutumwa abayo alikuwa amepatiliwa.

Kulikuwepo mwito ya kiungu kwa Agano la kale na Mpya, na yote, ikiwa ni Noa, Moise, Elia, Yohana mubatijazi, ao Paulo, haijalishi ni nani, wote walikuwa na kutumwa kwa kiungu na itimiza.

Agano Jipya ilianzana na Yohana mubatizaji akionekana kwa wakati ulio wekwa, nikusema ni kipande cha wakati unabii wa Biblia ulikuwa ukitimilika kwa kuja kwa kwanza kwa Kristo. Yohana mubatijazi alikuwa na utume wa kiungu. Alikuwa mtu alietumwa kutoka kwa Mungu akiwa na mwito wa kiungu na kutayarisha jiya ya BWANA kama vile ilivyo tangazwa katika Isaya 40:3 na Malaki 3:1 katika Agano la kale. Ageweza kurejelea Neno na kuitegemea kuwa ushuhuda wake.

Katika injili ya Yohana, katika sura ya kwanza, aliulizwa:

"*Wewe u nani? Naye alikiri, wala hakukana; alikiri kwamba, mimi siye Kristo. Wakamwuliza, ni nini basi? U Eliya wewe?"* (19-22) Na hapo alipana jibu lake kwa shahili ya 23. Hapo alirejelea neno hilo la Isaya 40:3: *"Sauti ya mtu aliaye, Itengenezeni nyikani njia ya BWANA; Nyosheni jangwani njia kuu kwa Mungu wetu."*

Kupitia hudma yake watu waliwekwa tayari, wametayarishwa kwa BWANA*: "Na wengi katika Waisraeli atawarejeza kwa BWANA Mungu wao. Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya, na nguvu zake, ili kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na kuwatilia waasi akili za wenye haki, na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa."* (Luka 1:16-17)

Ni nini kinacho tokea katika wakati wetu?

Ujumbe ambao William Branham alitangaza imeleta watoto wakweli wa Mungu kurundilia imani ya halisi ya mababa wakimitume.

BWANA Mungu ameweka macho yake juu ya Neno lake la milele. Lazima isemewe kwa sauti kubwa na wazi: ikiwa tugelijuwa yale ambayo Mungu amefanya nini hapo zamani Lakini hatujuwe yale alie ahidi na anayo ifanya leo mbele ya Kurundi kwa Yesu Kristo, tugelikuwa nafaida gani? Kulikuwepo mwito wa kiungu kwa wakati wetu pia; Ndugu Branham alikuwa anaweza kupana ushuhunda kwa hiyo tena na mara tena. Hapa kuna moja za nukuu zake kuhusu tukio ya siku la 11 Juni 1933, huko Jeffersonville: **"Nilisikia**

ikisema tena, Tazama juu! Na wakati nilipo tazama juu, haya kukakuja guzo ya Moto ile ambaye iliogoza wa Israeli jagwani. Maelfu ya macho iliiona ikikuya ikishuka chini hapa nilipo simama. Nakusema, «Kama vile Yohana Mubatijazi alivyo tumwa kutangulia kuja Kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utafunika Dunia na kutangulia kuja kwa Pili kwa Kristo.»" (Aprili 12, 1964)

Hiyo kwakweli njo ilifanyika ulimwenguni pote baada ya kufa ya Ndugu Branham; ilisha kuwa ukweli wakiungu.

Tayari kwa Juni, 12, 1958, Ndugu Branham iliniambia huko Dallas, Texas, "Ndugu Frank, utarundi Ujerumani na Ujumbe huu."

Imefikia utimilifu. Mungu amefanya yote mawili: Alitoa utume kuleta Ujumbe na pia alihakikisha kwamba ihubiriwe Duniani pote. Vitu vya Kibiguni vilifanyika maishani na hudma ya William Branham, sio tu Juni 11, 1933, Wakati alivyo fanya ubatizo wake wa Kwanza, alakini pia na mumikutano yake.

Mtume Paulo angeweza kushuhudia kwamba hiyo Nuru ilionekana kwake wakati alipo pokea mwito wake. Tuna abiwa katika Matendo 9: *"Hata alipokuwa akisafiri, ikawa anakaribia Dameski; ghafula ikamwangaza kote kote nuru kutoka mbinguni. Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, Sauli, Sauli, mbona waniudhi? Akasema, U nani wewe, BWANA? Naye akasema, Mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe…"* (Shahili. 3-5)

Paulo alishuhudia akiwa mbele ya Mfalme Agrippa na watu wanaotambulika zaidi*: "Basi katika kazi hiyo nilipokuwa nikienda Dameski, mwenye mamlaka na maagizo ya wakuu wa makuhani; Ee Mfalme, ndipo wakati wa adhuhuri njiani naliona nuru inatoka mbinguni ipitayo mwangaza wa jua, ikinimulikia mimi, na wale waliofuatana nami pande zote. Tukaanguka nchi sote, nikasikia sauti ikisema nami kwa lugha ya kiebrania, Sauli! Sauli! Mbona waniudhi? Ni vigumu kwako kuupiga mateke mchokoo. Nami nikasema, Wewe u nani, BWANA? BWANA akaniambia, Mimi ni Yesu, ambaye wewe unaniudhi. Lakini inuka, usimame kwa miguu yako, maana nimekutokea kwa sababu hii, nikuweke wewe uwe mtumishi na shahidi wa mambo haya uliyoyaona, na wa mambo ambayo katika hayo nitajidhihirisha kwako…" (*Matendo 26:12-16)

Tayari katika ya Agano la Kale, Uwepo wa Mungu was kiajabu ulijidhihirisha katika kichaka kinacho waka mto wakati Musa alipo pokea mwito wake. Musa alipashwa vuwa viato vyake kwa sababu alikuwa akisimama pahali patakatifu. Pale ndipo alitumwa na Mungu pekee (Kutoka 3).

Kwa Agano la Kale, BWANA Mungu alijifunuwa kupitia Nuru ya Nguzo la wingu na Nguzo ya moto.

Katika Kutoka 13 tunasoma: *"BWANA naye akawatangulia mchana ndani ya wingu mfano wa nguzo, ili awaongoze njia; na usiku, ndani ya moto mfano wa nguzo, ili kuwapa nuru; wapate kusafiri mchana na usiku…"* (Shahili 21) Sio ajabu? BWANA Mungu hakutosha watu Wake wa Israeli kwa utumwa tu, inje ya misri, lakini alitembeya mbele ya wenye ameita kutoka, wakombolewa, wenye amefanya Agano nao. Ali waongoza na kuwaongoza na kuwaonyesha njia mchana na usiku. Kwa hiyo miaka makumi inne (arobaini) ya safari yao, Alikuwa na watu wake-katika nguzo ya wingu ya kibinguni kwa mchana na katika nguzo ya mto kwa usiku. *"Ile nguzo ya wingu haikuondoka mchana, wala ile nguzo ya moto haikuondoka usiku, mbele ya hao watu."* (Shahili 22)

Hii inaelekezwa tena katika zaburi 78, shahili la 14*: "Akawaongoza kwa wingu mchana, Na usiku kucha kwa nuru ya moto."*

katika Kutoka 40 tuna soma: "*Basi Musa akaimaliza hiyo kazi. Ndipo lile wingu likaifunikiza hema ya kukutania, na huo utukufu wa BWANA ukaijaza maskani…Kwa maana lile wingu la BWANA lilikuwa juu ya maskani wakati wa mchana, na mlikuwa na moto ndani yake wakati wa usiku…* (Shahili 33b-34+38)

Wakati kila kitu ambacho BWANA alio angiza Musa kufanya kilitimizwa, utukufu wakimaajabu wa Mungu ulikuja kwa pahali patakatifu zaidi, kwenye kulikuwa saduku ya Agano na kushuhudia uwepo wa Mungu katika watu wake.

Wingu la kimaajabu ilishuka kwa mlima wa kubadilishwa, "…*Sauti ikatoka katika lile wingu, huyu ni mwanangu, mpendwa wangu, msikieni yeye*." (Marko 9:7; Mathayo 17:5) Katika Isaya 4:5 tunasoma yale anayo fanyikana wakati BWANA atamalia kazi yake kwa mlima wa sayuni: Ile wingu yakimaajabu litakuja tena, na uwepo wa Mungu

utaonekana waziwazi: *"Tena juu ya makao yote ya mlima Sayuni, na juu ya makusanyiko yake, BWANA ataumba wingu na moshi wakati wa mchana, na mwangaza wa miali ya moto wakati wa usiku; kwa maana juu ya utukufu wote itatandazwa sitara"*. Niyeye yule kila wakati: jana, leo, na milele.

Ripoti ya mushuhuda wamacho

Nina sema hii kama mushuhuda aliejionea na kusikia katika eshima mbele ya BWANA: Kama vile ninavyo njua, Nilikuwa na bahati la kuwa katika mkutano kadhaa ya Ndugu Branham. Alipo ombea wagonjwa, alikuwa akisema Mara na Mara, "Sasa hiyo Nuru la kibinguni, Sasa Nguzo la mto iko juu ya huyu mtu na huyo". Hata maelezo fulani juu ya mtu huyo mwenye ageombea ilimufunuliwa. Katika miaka mingi katika hudma yake, aliweza kusema zaidi yamara elfu "HIVI ASEMA BWANA…"

Siku ya Januari, 20, 1950, wakati Ndugu Branham alikuwa akihubiri kwa coliseum kubwa katika muji ya Houston, Taxes, kulikuwa watu zaidi elfu nane wenye wakulikuwa wanakusanyika hapo. Alipo ongeya, wale mpiga picha wa Press James Ayers and Ted Kippermann walimpiga picha zake. Wakati wa maendeleo ya filamu, waligundua kuwa ni picha moja tu iliyogeuka, ambaye niess moja ya Ndugu Branham na Nuru ya kiujiza juu ya kichwa chake.

Mtu anayesimamia hati zaku shakiwa kwa FBI huko Washington, Dr. George J. Lacy, alichuguza Picha hiyo na kuadika kwa ripoti yake ya siku Januari, 29, 1950, ya kwamba Nuru ilikuwa juu ya mhubiri, isige kuwa hivyo Kamera isingeiweza kuishika. Mungu yeye mwenyewe amepana ushuda Mara na Mara.

Kwa Decemba, 1962, Ndugu Branham alihamia Tucson, Arizona, Kama vile aliagizwa na BWANA kwa siku ya Marchi, 1962. Na ilitimika kwa siku Febuari, 28, 1963, iOS wingu kubwa ya kibinguni ilionekana wazi wazi kwa Kila Mtu kwa anga la bluu. Katika ile wingu kubwa, ambayo ilionekana juu ya mlima Sunset, Ndugu Branham aliona wamalaika Saba, na hapo Mtu wa Mungu aliagizwa:

“Rudi kwa Jeffersonville, kwa sababu mihuri Saba itafuguliwa.“

Kwa kuwa imechapishwa kwa siku Aprili, 19, 1963, Magazine Science inayo julikana vizuri, waliweka picha hiyo la wingu kubwa mwenye ukurasa wa kifuniko. Life Magazine kwa siku ya Mai, 17, 1963, ilichapisha habari iliyo na Picha ya Wingu chini ya kichwa cha maneno “Na Gonga kubwa La Wingu la Siri“. Dr . James McDonald kutoka Taasisi ya Fizikia ya Atmospheric (Institute of Atmospheric physics) aliandika habari mrefu kuhusu hiyo lakini hakukuwa na maelezo ya hayo. Bado ninayo magazeti yote mawili.



Kutabuwa siku na ujumbe

BWANA wetu aliochuga Neno lake na amekufanya kile kilicho patiliwa kwa hiki kipande Cha wakati. Na ahadi hii ametimilika kwa haki: *“Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya BWANA, iliyo kuu na kuogofya…“* (Malaki 4:5) Sasa tugali kwa siku ya wokovu (2 Wakorintho 6:2), kwa wakati ya Neema. BWANA wetu Yeye Mwenyewe aliabiya wanafunzi wake kwa Mlima wa kubandishwa, *“Akajibu akawaambia, Ni kweli Eliya yuaja kwanza, na kurejeza upya yote…“* (Marko 9:12) Mwito wamwisho inaedelea, na Yule alie wa Mungu atasikiliza Neno la Mungu takatifu na kuikubali Kama uhahali wa pekee.

Kwa bahati mbaya, inapashwa semeka ingawa ile Uwepo wa BWANA kwa watu wa Israeli, wengi kati wao walipoteya pamoja na mioyo yao,

ili Mungu alipaswa kuapa: *"Kama nilivyoapa kwa hasira yangu, Hawataingia rahani mwangu."* (Waebrania 3:11, Hesabu 14:23). Waliabudu masanamu na kunungunika.

Katika 1 Wakorintho 10, kutoka kwa Shahili la 1 hadi 4, Paulo alituonyesha Mambo ya kibinguni ambayo Mungu alifanya katika yao. Ku Shahili la 5 hadi 10 alifafanuwa makosa ambayo wa Israeli wali fanya na jinsi Mungu aliwaadhibu kwa ajili Yao. Sasa kunafata alifa: *"Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani."* (1 Wakorintho 10:11)

Katika wakati wetu vivyo hivyo haitakuwa na faa kwa Mtu yeyote kurejelea kwa kile ambacho Mungu amefanya katika hudma ya William Branham, Kama yiko mukuabudu sanamu na Mtu huyo na kutangaza kwamba sauti ya Mtu huyo ni "Sauti ya Mungu" na kusabaza mafundisho ya mbogo. Haeleweki ni mafundisho ngapi ya uwongo yanayosambazwa chini ya kumbukumbu ya nabii na Ujumbe. Wa moja yao wanasema kwamba nabii alifunua mambo ambayo haiandikiwe katika Biblia, kwa mufano kuhusu ngurumo saba. Yegine mafundisho isio ya kimaandiko inathibitisha kwamba ufufuo wa wafu utafanyika Kwanza na Kisha nabii atimize hudma yake maalum Kama vile "sahemu ya tatu" katika hema kwa muda ya siku 30 hadi 40. Kulingana na Wagalatia 1:8, kuko laana kwa watu Kama wale kwasababu wali hubiri injili engine (Ufunuo 22:18-19). Nabii yeye mwenyewe alirudilia na kusema, "Usikubali kitu chochote Kama hakiandikiwe katika Neno la Mungu."

Ndugu Branham pia alisema mara mingi, "Ujumbe ni: Rundi kwenye Neno, Rundi kwenye asili, Rundi mwanzoni, kumazoezi yenye waamini waliokuwanayo huko mwanzoni!" Siri zote zenye zilikuwa na fichwa katika Neno la Mungu zimefunuliwa; tu naamini hiyo. Hakuna, chochote kabisa kinaweza kuongezewa kwenye neno (Ufunuo 22).

Hakuna uwongo katika kweli (Yohana 2:21), na Yeyeto alie wa Mungu husikia kweli na kuamini neno la Mungu tu. Ni kweli kabisa Mungu mutakatifu hawezi kuweka mhuri yake kwenye mafundisho mabaya ao kumaisha ya wenye dhambi.*"Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli."* (Yohana 17:17)

Mtume Yohana aliandika kwa wale ambayo wali tabuwa ukweli*: "kwa ajili ya hiyo kweli ikaayo ndani yetu, nayo itakuwa pamoja nasi hata milele."* (2 Yohana 2). Amena!

Waasi wote na waongo watakuwa nje. *"Na ndani yake hakitaingia kamwe (munji takatifu- Yerusalemu mpya) cho chote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo."* (Ufunuo 21:27)

Acha Mungu awape neema kusudi kila mtu atabuwe yakwamba to tumefikia kipande cha wakiti ya mwisho, wakati ambamo mambo wote iliyopagiliwa na kuahidiwa kwetu katika Neno la Mungu inafanyika (Matendo 13:41). Acha kusikuwepo mmoja kati yetu wakuwa na moyo ya kutokuamini na kutotii. Kila BWANA wetu alisema juu ya Yerusalemu bado inatumika: *"Laiti ungalijua, hata wewe katika siku hii, yapasayo amani! Lakini sasa yamefichwa machoni pako."* (Luka 19:42) Anaita kutoka waliyo wake: *"Basi mambo hayo yaanzapo kutokea, changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia"*. (Luka 21:28)

Acha tuseme tena hii: wale wenye wako no moyo safi tu njoo wata muona Mungu. Wale tu wenye wako tayari joo wataitwa kwa arusi. Wale ambao wali ishi ukombozi kamilifu pamoja na upatanisho wakujaa tu na Kusamehewa na kubadilishwa upya, Wale tu mbao wa liishi kujazwa na kuwekwa mhuri wa Roho mtakatifu watafikia lengo.

Kwa mwisho ya ufafanuzi hii, kila mtu tena ukumbushwe kabisa juu ya kile ambacho BWANA wetu alieweka mkazo katika Matayo 17, shahili 11: *"Ni kweli Eliya yuaja kwanza, na kurejeza upya yote."* (Marko 9:12). Baada ya hudma ya Yohana mubatijazi, BWANA wetu alirudilia yale ambayo aliandikiwa katika semu ya pili ya ahadi ya mwisho katika Malaki 4:6: Yakwamba kupitia hudma ya Eliya, mioyo ya watoto wa Mungu igepashwa kurudi mara mmoja kwa imani ya wa baba yao Mitume.

Leo tunaweza kushuhudia: Andiko ilitimia; kile ambacho BWANA wetu alisema kilimefikia utimilifu. Kila fundisho la kibiblia limerudishwa, yakwanza na lamuhimu ni Uwungu, nikusema Mungu hafanywe na watu tatu wa milele, alakini alijifunua Yeyemwenyewe kama Baba katika Mwana na kupitia kanisa kama Roho Mtakatifu. Zaidi ya hao, Ubatizo wa maji wa kibiblia katika Jina la BWANA

Yesu Kristo kwale ambao wame kuwa awaamini (Matendo 2:38-41) ime rudishwa. Ujumbe wamwisho imeweka kilakitu kwa musingi halisi ya mitume na manabii, kwenye Yesu Kristo Yeyemwenyewe ni jiwe kubwa la pebe.

Mungu wetu amefanya mambo ya ajabu, na sasa tuko karibu kwa kumalizia ya kile ambacho kimefanyika mbele ya Kurudi kwa Yesu Kristo. Tuna Mshukuru Mungu kwa hao katika Jina la Yesu Takatifu. Amena.

Kwaheri kwa masafari ya kilamwezi ya kimishonanari

Katika myaka mingi, Kwa ujumla niweka kando wiki mbili za kila mwezi kwa safari za umishonari, kwa hiyo namna likuwa katika Zurich kwa mkutano kwa jumapili la mwisho, na katika Krefeld kwa wikendi ya kwanza. Kwa ujumla, Nilitumikisha maili ya milioni 15 za ndege katika mchakato. Vile, Niliweza kuhubiri katika miji mingi katika inchi 165 kwa Dunia yote.

Sasa Ni mefikia miaka 86, Igawa niko ndani ya uzima mzuri, miaka yangu imesimamesha kutembea, kuona, na kusikia, ni kusema safari murefu haziwezi wezekana. Igawa, kupitia mtandao, waamini wote kwa inchi zote wana weza kusikiliza mahubiri katika lugha tofauti na kushuhudia mkutano. Kwa jiya hiyo, uagalizi wakiroho kwa dunia yote imewezekana, kama vile waamini kutoka mudunia zima wanashuhudia na kushukuru.

Nina weza kusema: BWANA, acha sasa mutumishi wako eede kwa salama, kwasababu Ujumbe yamwisho imetanganwa ku Duniani yote. Macho yangu ameona utimilifu wa ahadi ya kipende cha wakati hii. Waamini wote wakweli wataishi kila kitu ambacho Mungu atafanya, mpaka mwisho. Aliahidi na ataitimiza.

Sana sana wale ambao walijiuga nasi kwa miaka kidogo iliopita kutoka ulimwenguni, Nina pendezwa ni wajulishe kwa machache kuhusu habari ya maisha yangu ya kiroho: Nilikuwa mhubiri katika kanisa la wapentekoste kutokeye mwaka wa 1952.

Wakati yangu yakwanza ya kukutana Ndugu Branham akwa, recepushioni ya hoteli kwa suku ya Juni, 15, 1955, Nabii aliniambia, “Uko mhubiri ya injili,“ akaonye kidolechake kushoto na kusema,

“Mke wako anasimama hapo kwa kiigilio“. Hapo kapatiana mikono na tukaogeya kwa machache. kutoka mwaka wa 1958 kuedelea, Nilitafusiri mahubiri za Ndugu Branham kwa lugha ya kijerumani.

Tarehe Aprili, 2, 1962 BWANA Yeyemwenyewe akanipa Utume kupitia sauti yake yaajabu ya kuhubiri Neno katika miji yegine.

Hapo, Nilikuwa na mazugumuzo mlefu pamoja na Ndugu Branham siku ya Desemba, 3, 1962, ambao ilishuhudia kutumwa kwangu kupitia Ufunuo mbele yawa shuhunda wawili. Kisha, akaniomba kuhumbiri munafayake huko Los Angeles kwa Demos Shakarian na pia huko Earnest Hotton katika Oakland, Oregon. Akaniomba nitembelea Ndugu Henry Martin huko Edmonton, Canada, ikiwazekana, nafasi kwenye kanda zake za mahubiri zilikuwazinasikiwa. hapo akanipa manjina na nambari za wandugu. Kwa mwisho yamaogezi, aliniambia, “Ndugu Frank, kama unashika safari ya umishonari kwa India, uite Paul Lawrie. Alikuwa katika mkutano yangu huko Bombay, ni muinjilist na alikuja huku Amerika na kubatiziwa hapa kwe hekalu katika Jina la BWANA Yesu Kristo.“

Katika mwaka wa 1964, Nilifanya safari yangu yaumishonari huko India. Huko ninashuhudia namna maelfu za watu walikuja kwa mkutano, na karibu waamini miatatu walibatizwa nyuma ya mahubiri. Kwa njia yangu yakurudi, Ni katembelea Yordani na Israeli.

Kufarikini kwa Ndugu Branham kwa mwaka wa Desemba, 1965, kipande cha wakati wamuhimu kilifikia mwisho. Semu mpya ikaanza, na utangazaji wa Ujumbe ya Neno kuligana na kutuma kwa Mungu kwa dunia yote, kwanza ni katika Ujerumani, Austria, na Uswissi, Ulaya yote na nyuma Dunia yote. Kwa kuogeza kwa mahubiri katika mikutano ya kuambundu na mkutano, Ni tumikisha kila muda kwa utangazaji ya Neno lililofunuliwa kupitia Ma redio na ma televisheni, na kupitia Mabaruwa Zamuzunguko na ma brosha.

Kwa mazishi ya Nabii sikua ya Aprili, 11, 1966, Nilialika Ndugu Pearry Green kukuja na kushuhundia kile ambacho aliona na macho yake katika hudma ya Ndugu Branham na alikuwa nashuhudia katika mkutano. “Katika ono, ambao nabii aliona ya calenderi na yakusimamia kwa mwaka wa 1977. Ilitaganziwa yakwamba kilakitu kitamalizika kwa mwaka 1977 na unyakuo utagefanyika.“

Nilikuwa mutafurisi wake na nikatamu maneno kuhusu ile kalenderi katika Baruwa yangu yakwanza ya Muzunguko kwa mwaka wa 1966. Nyuma nikaguduwa yakwamba Ndugu Branham hakuongeyaka kuhusu kalenderi.

Wakati mwaka 1977 ilikuja na kupita, fundisho mpya ilitangazwa yakwamba ufufuo utafanyika kwa ilewakati wa mutikito kubwa ambao itapiga magalibi ya Amerika, na Nabii atamalizia hudma yake katika hema. Hakuna mwenye anaweza zihusisha na ile Mafundisho yote ya uwongo-nikupoteza muda.

Bila kuigia kwa katika maelezo kuhusu somo hizo ambazo ziletwa na wa hubiri wa kutoka Amerika, Hii inastahili kusemewa: Hakuna katikati yao mwenye anaweza kutuonyesha kutumwa kwake. Hakuna katikati yao ambaye anahubiri Neno; wote walifundisha madithi zao ambazo walitayzlisha, na wote walifulahia ma Nukuu: “Nabii alisema…“

Hii ninaisema kwa Utukufu wa Mungu: Sijawai kuweka kando Neno na kuikubali tafusiri. Hiyo ilifanya wandugu wanipiganisha kwasababu wanaweka manukuu za Ndugu Branham juu ya Neno na Hawa kukubali Neno lilioandikwa kuwa Mamlaka ya mwisho.

Kulifika mwaka wa 1979, wakati adui alipanda mashaka kuhusu kutumwa kusundi anifanye nisitumainiwe na kubomoa kanisa. Nilikuwa kwenye mzabaho kwaghafla, kidongo kufikia mwisho ya mahubiri, Mke akaletakelele kwasauti kubwa, “Kilakitu hapa ni ujaja! aokeni inje, muache Jengo hii, na musirundi apa tena, kwasababu Kilakitu hapa kinamalizika milele!“ Yeyote aliye amini maneno ya Sauti ya ule mke hajawaii kuingiya tena kwa Jengo hii mpaka Leo. Wale ambao wana amini kile Sauti ya BWANA alisema siku ya Aprili, 2, 1962, na Ndugu Branham akaiakisha tarehe Desemba, 3, 1962, mbele ya washuhuda wawili, wanajuja wakitoka ku Dunia yote na kujaza Jengo la Kanisa. Na maelfu za watu wanajiuga nasi kupitia mtandao na wasikia Neno takatifu yahii wakati. BWANA hukaa macho kwa Neno lake na hakukubalia yule adui kubomola kazi yake.

Sehemu yapili ya kutumwa kuliopewa kwa tarehe Juni, 11, 1933, Nikusema Ujumbe itachukuliwa Duniani pote, ilitimilika machoni petu. Katika Mathayo 24:14, BWANA wetu alisema Yeyemwenyewe:

“Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja“.

Ndugu Branham aliagizwa katika Marchi 1962 kuweka chakura kwenye maweko, Kama vile alibisema tarehe Aprili, 1. Wakati alipokuwa aniongelea kuhusu muhuri ya Saba, aligeukia Ndugu Neville badala ya dakika kumi na kusema, “Kwasa chakura imekwa kagalani.“ Kwa tarehe ya Jumapili, Septemba, 1976, BWANA aliogea na mi kwa Sauti kubwa: “Mutumishi Wangu, nilikutaalisha kulingana na Mathayo 24, Shahili la 45 mpaka 47, kupana Chakura Kuwakati inayo faa.“ Nime patia wandugu wote katika hudma na watu wa Mungu. Wachaguliwa wote wanaamini kila Neno la Mungu na kueshimu maamzi Yake. Wanakulia kwenye mza ilioandaliwa ya utajiri ya BWANA.

Niko mtu pia kama Elia, Paulo, ao Ndugu Branham, alakini nikweli tena yakama nime chukua kutumwa kwahapohapo ambao BWANA ilinipa. Hakuna sababu yakurudilia mashuruti na mazoefu ambao BWANA muaminifu alionipa katika miaka yote. Nime kwisha kuongelea hao katika mabaruwa zamuzunguko tofauti.

Kila zoefu la kibinguni ni kweli; Mungu ni mushuhuda Wangu. Kama vile Paulo na Ndugu Branham, Ninaweza kusema saa na nafasi kwenye nilipata hayo.

Kwa neema ya Mungu, Ninaweza kushuhudia kama vile Paulo niliitwa, *“aliyeitwa kuwa mtume, na kutengwa aihubiri Injili ya Mungu; ambayo Mungu amekwisha kuiahidi kwa kinywa cha manabii wake katika maandiko matakatifu“* (Warumi 1:1-2) nani mechukua kutumwa yangu. Kulingana na wafilipi 1:6, BWANA Yeye mwenyewe atamaliza kazi yake: *“Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu.“*

“Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la BWANA kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema BWANA wa majeshi.“ (Zekaria 4:6)

Katika huduma Yake,

Ma alama za nyakati

Tunaishi katika utimilifu wa unabi wa kibilia. Mabadiliko ya Hali ya hewa ni alama ya nyakati ya mwisho. Ilikuwa imetabiliwa, na zinazohusiana na taifa la Israeli pamoja na kurudi kwao kwenye Inchi ya Ahadi.

Tuone karibu yale amboyo Mungu alitangaza kupitia Nabii Isaya kwa sura ya 30 na kwa shahili ya 26:

"Na tena nuru ya mwezi itakuwa kama nuru ya jua, na nuru ya jua itaongezeka mara saba, BWANA atakapofunga mapigo ya watu wake na kuriponya pigo la jeraha yao"

Badiliko ya hali ya hewa na ogezeko la joto duniani inafanyika kupita myale ya jua ingepashwa kuwa mwito ya kuamisha kwa watu wote? Tetemeko la inchi na mambo yamengine ya ajabu ya kimbingu yanaendelea kuonekana hapo na pale, Lakini badiliko la majina ni Duniani pote.

"Hilo ndilo kusudi liliyo kusudiwa duniani mwote na huo ndio mkono ulionyoshwa juu ya mataifa yote. Maana BWANA wa majeshi amekusudia, naye ni nani atakaye libatili? Namkono wake ulionyeshwa, ni nani atakaye ugeuza nyuma?" (Isaya 14:26-27)

Watu wote duniani wanajua kwamba badiliko la hali ya hewa ya anga na ongezeka la joto ya endelea na wote hutafuta suluhisho bila matumaini. Mambo ya ulimaji inayo tupatia chakula, nayo vile vile imeguswa. Na hii itasababisha njaa ulimweguni pote. Igawa kuko maandamano na mipago ya kupungaza uzalishaji wa Carbonoxide (CO2), unabii ulio andikwa katika maandiko kwa wakati huu utatimilika.

Maandiko ya Biblia inaonyesha wazi wazi kwamba ongezeko la mionzi la jua litaongezeka mara saba kwa siku, na inaambatana na kurundishiwa ya uharibifu ambao umefanywa kwa Israeli.

Jemadari wa Warumi Titus alibomoa hekalu na Ku Kusambaza Yelusalemu Kwa mwaka wa 70 Nyuma ya Yesu Kristo na wa Yuda Wakatawanyika Katika duniani pote. Kwa wakati wa Constantine, wakati Kanisa la Jimbo la Roma lilipo umdwa chini ya Athanase, kwa mwaka wa 321 nyuma ya Yesu Kristo, Ilikuwa inakataziwa Kwa wa Yuda Ku shiriki sabato na Masinagogi ziligeuzwa Kuwa Manyumba

za Ngombe. Kwa wakati ule ukiritimba wa ukristo ulitokea na leo unafwatiliwa.

Wayahudi wali teseka vibaya sana sana Kwa wakati wa ukwazadi saba zilizo amriwa na mapapa; Wayahudi walipigwa na mateso makubwa. Mwito ulikuwa ,“kulipaza kisasi kwa damu ya Yule aliyesulubiwa“. Ukiwazaidi wa kwanza ulidumu tangu 1069 mpaka 1099 uliyo fanya mavaji ya wayahudi 70,000 vile vile na mataifa mengine ya mwisho ili anza kwa 1248 mpaka 1254 hesabu yote kwa ujumla ambayo ili uwawa haijulikane vizuri, kwa kukadilisha hatujuwe kama kulikuwa mamiya ao millioni moja tangu wakati wa dhabihu na shoah, kulikuweko millioni sita (6).

(PHOTO]

Tuyarudilie: Ongezeko la joto la jua mara saba, kama vile ilivyo tabiriwa na kwamba inaambatana na kuridi kwa taifa la Israeli kwenye Inchi ya Ahadi. Selekali ya Israeli ilionekana tena upya tangu siku 14 mei 1948 na gunvu ya kuweza kufanya makubaliano ya amani ya inchi za mashariki ya kiti, inafikiya hatuwa yake kubwa. Vidonda vilivyo patikana kwa taifa ya Israeli vimo vinaaza kupona.

Wakubwa: (viogozi vya selekali) wange weza kuheshimu maadiko yenye imeandikwa kwa katika, hati ya dhamana yani Biblia/torah. Katika maneno hayo munano kuhusu Yerusalemu na Mlima wa Hekalu.

Kulingana na Mwanzo 22, Ibrahimu aliagizwa kumtoa mwanawe Isaka kama dhabihu kwenye Mlima Moriya, kuna pita karibu mwaka 4000, Mlima huo ndio uliyo geuka kuwa Mlima wa Hekalu:

"Kasema umchukue mwanao, mwana wako wa pekee umpendeya Isaka ukaenda zako paka inchi ya moriya, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmoja wopo ritakapo kwambia". (shahili la 2).

Kufwatana na 1. Mambo ya Nyakati 21:18-25, Daudi alinunua dongo kutoka kwa Ornan mu Nyebusi: *"Ndipo huyo malaika wa BWANA akamwamuru nabii Gadi kwamba amwambie Daudi, yakuwa Daudi amkwee akamwinulie Bwana madhabihu katika kiwanja cha kupuria cha Arauna nyebusi … Basi Daudi akampimia Arauna thamani ya mahali pale Shekeli mia sita za dhabihu kwa uzani."* zinazo lingana kwa sasa karibu na 600,000 euro ao Dola 660,000.

Kulingana na 2. Mambo ya Nyakati 3, Sulemani ilijenga Hekalu juu ya Mlima Moriya-Mlima wa Hekalu: *"Ndipo Sulemani akaanza kuijenga nyumba ya BWANA huko Yerusalemu, juu ya mlima moriya, pale BWANA alipo mtokea Daudi badaye alipotengeneza mahali pale alipoagiza Daudi, katika kiwanja cha kupuria cha Arauna myebusi."* Ninaomba Heshima Mungu-Elohimu na Neno lake, Biblia/Torah.

Tuna washuhuda watatu walio chaguliwa na Mungu: Ibrahimu, Daudi na Sulemani wa nao semwa wakiabatanishwa na Yerusalemu na Mlima wa Hekalu. Maandiko haya matatu yanashuhudia kwamba hakuna mtu hata mwengine anaye kuwa na luhusa ya kusamba kuhusu Yerusalemu na Mlima wa Hekalu.

Acheni tuangalie kwa maandiko machache yanayo sema kuhusu kurudi kwa taifa la Israeli. Ukweli hauwezi kukataliwa na mtu yeyote.

"Maana BWANA atamhulumia Yakobo, atamchagua Israeli tena, naye atawaweka katika inchi yao wenyewe, na mgeni nyumba ya Yakobo." (Isaya 14:1)

"…Ee bikira wa Israeli irudie hii miji yako." (Yeremia31:21b)

"*Na BWANA atairithi Yuda, iwe sehemu yake katika inchi takatifu, naye atachagua Yerusalemu tena."* (Zekaria 2:12).

"Hakika BWANA Mungu hata fanya neno lolote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake" (Amosi 3:7).

"Inchi iliyokuwa ukiwa italimwa, ijapokuwa ilikuwa ukiwa mbele ya macho ya watu wote walio pita. Nao wa tasema nchi hii iliyo kuwa ikiwa, imekuwa kama bustani ya Edeni nayo miji iliyo kuwa mahame na ukiwa na magofu, sasa ina maboma, inakaliwa na watu" (Ezekieli 36:34-35). Maandiko haya yote yametimia machoni petu.

Katiki nabii Ezekieli, sura 47, kujengwa tena kwa Hekalu kumeandikwa na uhakika kwa sura 48, tunaoneshwa kabila 12 za Israeli katika inchi yao, kulingana na Yosua aliwagawiya, kama vile ginsi Mungu alipanga kwa wale ambao wamegawa Israel, hukumu imetangazwa juu yao:

"*Nami nitawaleta chini katika bonde ya Yehoshafau na huku nitawahukumu kwa ayili ya watu wangu Israeli ambao wamewatawanya kati ya mataifa na kuigawanya nchi yangu"* (Yoeli 3:2b).

"Tena itakuwa siku hiyo nitafanya Yerusalemu kuwa jiwe la kuwalemea watu wa kabila zote, wotu watakao jitwika jiwe hilo watapata jeraha nyingi, na mataifa yote ya dunia watakusanyika pamoja juu yake" (Zekaria 12:3).

Hakuna hata mtu mmoja anaye weza hata kuzuia yale ambayo yametabiliwa katika unabii wa kibilia kwa wakati huu.

"Tena, tutakuwa na ishara katika jua, na mwezi, na nyota, na katika inchi dhiki ya mataifa wa kishangaa kwa unvumi wa bahari na musukosuko wake (Luke 21:25).

Kwa sasa yale yote yaliyo tabiriwa kwa unabii wa wakati wa mwisho kuhusu Israeli uko unafanyika. Badiliko la Anga na ongezeko la joto la u jua, hiyo inatuonayesha wazi wazi kama alama ya nyakati. Yale

ambayo nabii Isaya, aliyo yatabiri, yanadumu ya kweli na tunaweza kusema kwamba maandiko haya yanatimia machoni petu.

Mungu wa Israeli anatengeneza shida zilizo pata taifalake, na kutunza vidonda ambavyo walivyo vipata (Isaya 30:26). *"Lakini heri macho yenu, kwakuwa yanaona, na masikio yenu kwa kuwa yanasikia!"* (Mathayo 13:16).

"Naye BWANA atangwuma toka sayuni, atatoa sauti yake toka yerusalemu, na mbingu na nchi zitatetemeke, lakini BWANA ata kuwa kimbilio la watu wake, Ngome ya wana wa Israeli. Hivyo ndivyo mtakavyojua ya kuwa mimi ndiye BWANA, Munguwenu, nikaaye sayuni, mlima wangu mtakatifu, ndipo yerusalemu utakapo kuwa mtakatifu, wala wageni hawatapita tena ndani yake kamwe" (Yoeli 3:16-17).

"Katika siku hiyo BWANA atawalinda wenyeji wa yerusalemu, nay eye aliye dhaifu miongni mwao atakuwa kama Daudi siku hiyo, nayo nyumba ya Daudi itakuwa kama Mungu, kama malaika wa BWANA mbele yao" (Zekaria 12:8).

Hivyo ndivyo mataifa yote ya malizia kutambua.

Hevenu Shalom Alechem

****